

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA MJI MAFINGA



24/02/2023

**TANGAZO LA ZABUNI YA UKODISHAJI WA MGAHAWA PAMOJA NA  
DUKA KATIKA HOSPITALI YA MJI WA MAFINGA**

**A: UTANGULIZI**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga anawatangazia wananchi, wafanyabiashara, makampuni, vikundi vyote vyenye sifa na uwezo wa kukodi Mgahawa na Duka watume maombi yao kama ilivyoainishwa hapo chini:-

**B: ZABUNI YA UKODISHAJI WA MGAHAWA NA DUKA**

NA.	NAMBA YA ZABUNI	CHUMBA CHA BIASHARA
1.	LGA.169/2022/2023/NC/01	MGAHAWA
2.	LGA.169/2022/2023/NC/02	DUKA


**C. SIFA ZA MWOMBAJI**

1. Muombaji asiwe Mtumishi au Diwani wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga
2. Muombaji awe na umri usiopungua miaka kumi na nane
3. Muombaji awe na akili timamu.
4. Muombaji awe na Leseni ya biashara na namba ya utambulisho ya mlipa kodi (TIN)

**D: MASHARTI KWA MUOMBAJI:**

1. Muombaji atatakiwa kuandika barua ya maombi inayoainisha kiasi cha fedha atakachoilipa Halmashauri kwa mwezi, namba ya zabuni au chumba anachoomba kukodishiwa.
2. Muombaji asiwe anadaiwa na Halmashauri ya Mji wa Mafinga.
3. Waombaji wanaotaka kukodishiwa Chumba cha Mgahawa wanatakiwa kuambatanisha Mkataba wa Wakala wa Ununuzi Serikalini (GPSA) wa mwaka wa fedha 2022/2023 wa utoaji wa huduma ya Chakula katika taasisi za Serikali.

4. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe 13/03/2023 Siku ya Jumatatu, saa 4 kamili asubuhi. Maombi yote yanatakiwa yawe yamefungwa kwenye bahasha yenye lakiri na isiyo na alama ya kumtambulisha aliyeomba. Yanatakiwa yawe yameshatumwa kwa Register au kuletwa kwa mkono kwenye Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji wa Mafinga iliyopo eneo la Luganga, S. L. P. 76, Mafinga kabla na si zaidi ya saa 4:00 asubuhi tarehe 13/03/2023 na ufunguzi utafanyika mara tu mwisho wa saa na tarehe tajwa hapo juu kukamilika.
5. Kila atakayeomba ni lazima aonyeshe namba ya zabuni pamoja na chumba alichoomba juu ya bahasha na aonyeshe kwa maandishi isifunguliwe hadi tarehe 13/03/2023.
6. Vitabu vya Zabuni vinapatikana katika Jengo la Ofisi ya Mkurugenzi wa Mji wa Mafinga lililopo Luganga chumba Na. 12.
7. Tathimini itazingatia masharti yaliyoainishwa kwenye tangazo na kitabu cha zabuni husika.
8. Watakaoshinda zabuni hii wataingia mkataba wa upangaji na Halmashauri wa muda wa Mwaka mmoja.
9. Watakaokuwa wameshinda zabuni hii watatakiwa kulipa kodi ya miezi mitatu kabla ya kusaini mkataba, na kodi iliyobaki itakuwa inalipwa kwa mkupuo wa miezi mitatu na italipwa mwanzoni kwa kila mkupuo.
10. Ada ya maombi ya zabuni hizi ni shilingi za kitanzania Elfu ishirini tu (20,000) ambazo hazirejeshwi na zianapaswa kulipwa kwa njia ya mfumo wa kieletroniki baada ya kupata namba ya malipo (control Number) kutoka ofisi ya Mwekahazina wa Halmashauri ya Mji wa Mafinga kuanzia saa 1:30 asubuhi hadi saa 9:30 jioni siku za kazi, kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa. Kila zabuni utakayoomba malipo yake yanajitegemea.



**HAPPINES R. LAIZER**  
**MKURUGENZI WA MJI**  
**HALMASHAURI YA MJI WA MAFINGA**

**MKURUGENZI HALMASHAURI YA**  
**MJI - MAFINGA**